# "ULEMAVU BARANI AFRIKA "

# EPISODE 6: " MABADILIKO "

**AUTHOR: Chrispin  Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**List of characters / Episode 6:**

**MSIMULIZI**

**<u>SCENE ONE: AT FAGILIO'S HOME IN BACKYARD</u>**

- Fagilio (mume, 42)
- Chitoto (mume, 18)

**<u>SCENE TWO : SHOE REPAIR OUTSIDE OLUANDA'S HOME</u>**

- Oluanda (mume, 18)
- Kangwa (mke, 18)

**<u>SCENE THREE : DINNER AT OLUANDA'S HOME</u>**

- Tofa (mke, 40)
- Oluanda (mume, 18)

**<u>SCENE FOUR:NIGHT AT THE MALI'S HOME</u>**

- Kangwa (mke, 18)
- BW. Mali ( mume, 50 )
- BI. Mali ( mke, 45 )

**UTANGULIZI:**

Hujambo tena na karibu katika kipindi chetu cha leo cha ‘ Walemavu barani Afrika” **.** Kipindi cha tano kilichopita, Oluanda alimueleza mamake azma yake na msukumo wake wa kutaka kuwa mshona viatu ulitokana na nini.. kwengineko nako Fagilio alimgundua kijana wake, Chitoto alikuwa ameanza kupiga buruji. Sasa,kila mmoja anajuwa mabadiliko ni magumu kupatikana. Watu kweli wako tayari kukubali mabadiliko? Kaa karibu na redio yako tushuhudie ni mageuzi gani ambayo Oluanda ananuia kuyaleta katika Maganye. Lakini kwanza tumsikize Fagilio atasema yapi kuihusu tabia ya Chitoto ya kunywa pombe akiwa na umri ule mdogo.

**SCENE ONE : AT FAGILIO’S HOME IN BACKYARD**

**1. SFX: YARD AMBIENCE; BIRDS; PEOPLES NOISE FROM AFAR**

**2. FAGILIO:** Chitoto okota hiyo chupa, na unifuate ndani. Sasa hivi!

3. **SFX:** **BOTTLE ROLLS ON GROUND**

4. **CHITOTO:** Nisamehe baba...

5. **SFX:** **DOOR OPENED**

6. **FAGILIO:** Ingia ndani! Mkosa nidhamu, huna hata shukrani!

7. **SFX :** **FOOTSTEPS OF TWO PEOPLE (MAN, BOY)**

**ENTERING THE HOUSE**

8. **SFX:** **DOOR BEING CLOSED**

9. **FAGILIO:** Mara moja, usinifiche kitu Chitoto. Sijalewa leo, kwa hivyo usijaaribu kunidanganya. Uliuanza lini kunywa pombe? Kwanini mamake Oluanda kila wakati analalama kuhusu jambo fulani analofikiri umelitenda?

10. **CHITOTO:** Sawa , sawa baba. Kusema kweli nilianza kunywa baada ya ajali ya Oluanda…

**11. MSIMULIZI:** Watu wengi hufikiri kujizamisha kwenye pombe au vileo vyengine ndio matatizo yao huwakwepa au kuisha. Bila ya shaka Chitoto anaiga haya kutoka kwa babake akidhani kuwa ulevi wa kupindukia utamnusuru kutokana na kuhukumika kwake. Chitoto alimueleza babake, walivyoanza kwa kuekeana ahadi, alivyoanguka, ajali ilivyotokea hata Oluanda alivyopoteza mguu wake na kumpa hatima aliyonayo sasa. Fagilio alimtazama mwanae machoni kisha…

12. **FAGILIO:** **(Thoughtful))** Hmm… kwa hivyo
Tofa alikua anasema ukweli?

13. **CHITOTO:** Ndio. Nilijaaribu kukueleza mara nyingi kuhusu haya lakini hukunipa muda kwa sababu ulikuwa ima umlevi au unang’orota. Hata kuna siku ukafikiria nimempachika msichana mimba..

14. **FAGILIO:** Lahaula? Itanibidi niache kunywa . Sasa, Nisikize kijana wangu..ni lazima uache hii tabia.Sitaki uaharibikiwe kama mimi.Nimejitolea kwa mengi ili uwe na Maisha mazuri. Namaanisha, lazima utafute suluhu na Oluanda.Hakuna kitu kibaya kama kuishi kwa majuto.Wanisikia mwanangu? Kamtake radhi, haraka iwezekanavyo..

15. **CHITOTO:** Baba.. hiyo itakuwa ngumu kwangu…

16. **FAGILIO:** Sijali kama itakuwa ngumu nenda  katupe hiyo chupa haraka!

**17. MSIMULIZI:** Chitoto alisema kweli, kajipalia makaa mwenyewe. Kando na kuvunja urafiki wake na Oluanda baada ya ajali, rafiki zake wawili, Magoto na Karemi pia walichoshwa na udhalimu wake, hili pia alitambua vyema. Baada ya majuma kadhaa kupita, Oluanda alikuwa keshajulikana kama mshona viatu mashuhuri. Mchana mmoja akiwa katika harakati za amali yake, Kangwa, msichana mrembo zaidi shuleni alikokuwa akisoma

alikuja akitaka huduma za Oluanda, lakini hiyo ndiyo sababu pekee au kuna zaidi?

**SCENE TWO: SHOE REPAIR OUTSIDE OLUANDA'S HOME**

18. **SFX: OUTSIDE AMBIENCE; BIRDS; PEOPLE PASSING BY; GENTLE HAMMERING ON NAIL**

19. **KANGWA:** Oluanda, hujambo. unaendeleaje?

20. **OLUANDA:** **(Happy mood)** Ei! Kangwa, ni vyema kukuona. Tafadhali karibu ukaa……. mmh.. itanibidi niweke fomu ya watu kuketia hapa…

21. **KANGWA :** Usitie shaka. Nitasimama tu. **(Embarrassed)** Oluanda, viatu vyangu… kwa vile kila mmoja hapa Maganye anausifu umaarufu wako…namaanisha kuhusu ushonaji viatu.

22. **OLUANDA:** Hebu nione?

23. **KANGWA:** Bila shaka. Ndiposa nikaja hapa.. lakini sio hivyo pekee … pia nilitaka nijue unaendeleaje..

24. **OLUANDA:** Nashukuru kwa ukarimu wako Kangwa. Unavihitaji viatu vyako haraka? Kwa sababu nina kazi nyingi kwa sasa, lakini msichana kama wewe hafai kutembea bila viatu avipendavyo..

25. **KANGWA:** Eti msichana kama mimi? Sina tofauti na

wasichana wengine walioko hapa Maganye.

26. **OLUANDA:** Kama huna tofauti nao basi wao wana tofauti na wewe **.**
**(They both laugh heartily)**

27. **KANGWA:** Samahani kwa kukuuliza, lakini ungependa kufanya kazi hii maishani?

28. **OLUANDA:** Unazungumza kama mamangu. Lakini nitakujibu, najuwa ninachotaka kufanya, na sio kushona viatu, lakini sijui ni vipi, wapi, au lini nitaanza! Ndio nikaamuwa kuanza na hii,ili nisikose maana maishani.

29. **KANGWA:** **(Curiously)** Enhe! Mimi ni rafiki yako, naweza kukupa msaada… labda. Niambie Oluanda, ulikuwa mmoja wa wanafunzi bora, na nakumbuka ulikua ndoto kubwa maishani..

30. **OLUANDA:** Nikikueleza ndoto zangu, waweza kudhania sikupoteza mguu wangu pekee bali hata akili yangu.

31. **KANGWA:** **(Shocked)** Ati nini!?

32. **OLUANDA:** Usijali nakufanyia mzaha tu.

33. **KANGWA:** Kumbe..aah wewe Oluanda nawe!
**(Hearty laugh again))**

34. **MSIMULIZI:** Kangwa, msichana mrembo zaidi Maganye na Oluanda, walitaniana na kucheka kwa muda mrefu. Mwishowe Oluanda akamueleza ndoto yake, matakwa na mtazamo wake. Kangwa alipendezwa sana kwa msukumo na umahiri aliokuwa nao Oluanda licha ya hali yake. Wakaungana na kuwa na lengo moja.Lakini familia zao zitawachukulia vipi? Endelea kusikiliza. Wa kwanza kuzitoa habari hizi alikuwa Oluanda, lakini kwa Tofa haikumpa mshangao kwa sababu aliona tabasamu na ucheshi wa mwanawe walipokuwa mezani jioni.

**SCENE THREE : DINNER AT OLUANDA'S HOME**

35. **SFX : CUTLERY SOUNDS OF PEOPLE EATING**

36. **TOFA:(Teasing)** Enhe… Oluanda, sasa utanieleza saa ngapi?

37. **OLUANDA:** Mmh?... kukueleza nini mama?

38. **TOFA:** Wewe umwanangu? Nakujua alifu mpaka wassalamu. Macho yako yananieleza kunalo lakuniambia, sikumbuki ni lini nilikuona ukiwa na furaha jinsi hii..

39. **OLUANDA:** Hmm…

40. **TOFA:** Kumejiri nini? Nasubiri kwa hamu na ngamu, uniambie ni kitu gani kimekufurahisha hivi.

41. **OLUANDA:** Sawa , sio kitu.. ni kuhusu mtu..

42. **SFX: SPOON DELICATELY PLACED DOWN**

43. **TOFA:(Curiously)** Mtu? Haya nishatega masikio. Huyo mtu ni nani na amefanya nini?

44. **OLUANDA:** Umekosea tena mama, si mtu tu, ni msichana..

45. **TOFA:**Msichana? Aha kwa hivyo ni msichana. Haya ni nani? Amekupa bakshishi kubwa kwa kumshonea viatu vyake?

46. **OLUANDA:** **(satirically)** Ndio na hapana.

47. **TOFA:(Nervous)** Oluanda acha kunizungusha.. unamaanisha nini ndio na la?

48. **OLUANDA:** Ndio, amenipa bakshishi, Lakini sio ya pesa. Alinipa ari mpya ya ndoto zangu. Mama, niko tayari kufanya mabadiliko.

49. **TOFA:(Happy)** Oluanda, hizo ni habari njema! Hata mimi nimefurahi. Sasa unataka kurudi shule? Unajuwa unaweza kujiunga na shule ya ufundi au..

50. **OLUANDA:** Labda nitajiunga. Lakini sasa hiyo sio ndoto yangu pekee! Ndoto yangu ni kuwa walemavu wote wanaotaka kupata elimu wawe watapewa fursa hiyo…

51. **TOFA:(Puzzled)** Sasa unatarajia vipi kufaulu kuitimiza ndoto hii? Huyu msichana ni nani?

52. **OLUANDA:** Nitafaulu, au tuseme tutafaulu. Na hata tusipofaulu, itakuwa tumeleta changamoto na ushindi utakuwa wetu.

53. **TOFA:(More puzzled)** Sawa, huyo mwanamke anaitwa nani, nataka kuzungumza nayeye. Naona amekutia kasumba.

54. **OLUANDA:** Ni Kangwa. Ndio ni yeye.

55. **TOFA:**Oluanda,unanitatiza. Eti Kangwa? Yule msichana mrembo uliyemfukuza alipokuja kukutembelea ulipotoka hospitali?

56. **OLUANDA:** Huyo huyo, hakuna Kangwa mwengine.

**57. MSIMULIZI:** Kila mzazi atakuambia kuwa hutaka mtoto wake awe na furaha. Tofa hana tofauti. Alimsikiza Oluanda kwa makini akimueleza jinsi walivyokutana na binti mrembo wa Maganye. Mwishowe hakuwa na la kusema ila..

58. **TOFA:(Takes one long deep breath)** Sina la kusema? Furaha yako ni yangu. Bora kuwa mwangalifu, sitaki ukimbilie jambo alafu uje ujute baadae, la sivyo, uje kuvunjika moyo. Acha niondoshe vyombo, utanisaidia kesho.

59. **SFX: CUTLERY BEING COLLECTED**

60. **MSIMULIZI**: Wakati Tofa, akiondosha vyombo, alijiuliza maswali mengi kuhusu uhusiano wake na mwanawe, pia na watu wa Maganye. Alifahamu kuwa Kangwa anatoka katika familia ya "tutakula na nini" wakati wao wanatoka familia ya " tutakulani?", alijuwa hilo lingeleta shida. . je, aliwaza kweli? Wazazi wa Kangwa Bw na Bi. Mali, ndio waliokuwa na gari pekee hapo Maganye. Japo kuukuu lakini walikuwa nalo. Usiku huo Kangwa akiwasubiri ndani ya nyumba wao walikuwa garini wakiteta.

**SCENE FOUR: NIGHT AT THE MALI'S**

61. **SFX : OLD CAR COMES TO A HALT**

62. **BI. MALI:** Kila siku nakwambia tunahitaji gari mpya husikii?

63. **BW. MALI:** Na kila wakati nakujibu, hatuhitaji gari mpya ,wewe pia husikii.

64. **BI. MALI:** **(Annoyed)** Ni aibu kuonekana ndani ya gari lilojaa kutu kila pahala.

65. **BW. MALI:** Basi shuka utembee. Unastahili ushukuru; unajuwa ni wanawake wangapi wanaomba angalua wapate nafasi yako?

66. **BI. MALI:** Sasa yamefikia hapo? Yote haya ni kuhusu wanawake wangapi wanaotaka nafasi yangu sio?

67. **BW. MALI:** La,namaanisha nafasi ndani ya gari! Mama Kangwa. Gari linatusitiri…

68. **BI. MALI:** Hapana! Hili gari ni bovu! limezeeka huioni wewe ,kwani u kipofu nini?

69. **BW. MALI:** Sioni tatizo la gari hili.

70. **BI. MALI:** Tatizo liko!

71. **SFX: CAR DOOR IS BANGED HARD**

72. **BW. MALI:** Sasa ukiwa unalifunga hivyo litakuwaje zuri?

73. **SFX: FOOTSTEPS OF GIRL APPROACHING**

74. **KANGWA: (coming closer)** Shikamoo mama na baba..

75. **BI. MALI:** Marahaba. Umemaliza kazi za shule?

76. **KANGWA:** Kwani mulikuwa mwateta? , kazi nimemaliza, nilikuwa nawasubiri kuna jambo nataka kuwaeleza…

77. **BI. MALI:** Umesikia wewe? Kangwa anataka kutueleza kitu..

78. **BW.MALI:** Sawa, naja.

79. **SFX: CAR DOOR GENTLY CLOSED**

80. **SFX: FOOTSTEPS OF MAN, FOOTSTEPS OF WOMAN AND GIRL**

**HITIMISHO:**

Na haya yanatufikisha hatima ya kipindi cha sita cha tamthilia kuhusu “Ulemavu barani Afrika”. Mawimbi yanazidi kufura. Oluanda anapanga nini kuhusu haki za walemavu kijijini Maganye? Na je, itakuwaje wakati Bw na Bi. Mali, wazazi matajiri wa Kangwa, watakaposikia kuhusu uhusiano wa binti yao na Oluanda? Kwa hayo na mengine mengi ni kipindi kijacho. Unapotaka kusikiliza tena kipindi hiki u chengine kilichopita tembelea tovuti zetu www.dw-world.de/lbe.

Mpaka wakati mwengine. Alamusiki.